# TSN JARIDA

**Habari, Matukio na Maendeleo ya TSN**

Toleo Na. 1 | Maalum Mtandaoni| Juni 2026

tsn TANZANIA STANDARD NEWSPAPERS



## TSN na Historia Yake



**TSN yapiga hatua uwekezaji wa kisasa miundombinu ya uchapaji**



**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TSN IGP (Mstaafu), Said Mwema akiongoza kikao cha robo ya Tatu ya mwaka wa fedha 2025/2026 Tarehe 22 Mei 2026**



**TSN yashiriki Mei Mosi**

# TSN NA HISTORIA YAKE


DAILY NEWS

EAC ministers seal pact to boost regional trade, investment

Why Russia honoured Samia

PM calls for compliance with Ebola prevention guidelines

sundaynews

Why Samia's Russia visit reflects independent diplomacy, economic ambition

Samia elevates economic ties

Kwa takribani karne moja, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imeendelea kuwa nguzo muhimu katika sekta ya habari nchini kwa kuhabarisha, kuelimisha na kuunganisha jamii kupitia maudhui yenye kuaminika na huduma mbalimbali za mawasiliano ya umma. Ikiwa ni taasisi yenye historia ndefu na mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa, TSN imepitia mageuzi mbalimbali ya kiutawala, kiteknolojia na kimkakati yaliyoifanya kuendelea kuwa sehemu muhimu ya safari ya maendeleo ya Tanzania.

Historia ya TSN inaanza mwaka 1930 ilipoanzishwa chini ya umiliki wa East Africa Consolidated Holdings. Mwaka 1961, Taasisi hiyo ilinunuliwa na Lonrho London ambayo iligawanywa katika makundi mawili yaliyofahamika kama Tanzania Standard (Newspapers) Limited na Printpack Tanganyika Limited (PTL).

Hatua muhimu zaidi ilifikiwa mwaka 1970 wakati Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipoitaifisha kampuni hiyo na kuifanya kuwa mali rasmi ya Serikali ya Tanzania. Baada ya hatua hiyo, TSN iliendelea kuchapisha gazeti la "Daily News" pekee, ambalo limeendelea kuwa moja ya magazeti kongwe na yenye heshima kubwa nchini.

Gazeti la "Daily News" ambalo toleo lake la Jumapili hufahamika kama "Sunday News" limeendelea kuwa chanzo cha habari za kuaminika kuhusu masuala ya kitaifa na kimataifa, uchumi, biashara, siasa, uwekezaji na maendeleo ya jamii. Kwa miaka mingi, gazeti hilo limejijengea heshima kubwa kwa kutoa taarifa sahihi, uchambuzi wa kina na maudhui yanayochochea maendeleo ya taifa.

Katika jitihada za kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata habari kwa lugha wanayoielewa kwa urahisi, TSN ilianzisha gazeti la "HabariLEO" ambalo toleo lake la kwanza lilichapishwa Desemba 21, 2006. Uamuzi wa kuanzisha gazeti hilo ulitokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2005 – 2010 iliyolenga kuanzishwa kwa gazeti la Serikali kwa Lugha ya Kiswahili. Kifungu cha 116 (C) cha ilani hiyo kilisisitiza umuhimu wa Serikali kuanzisha gazeti la Kiswahili ili kuongeza upatikanaji wa habari kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa gazeti hilo uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM mjini Dodoma, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete alisisitiza umuhimu wa gazeti hilo kuzingatia ukweli katika utoaji wa habari, akieleza kuwa "HabariLEO" linapaswa kuandika "habari za kweli, ukweli mtupu hata kama unauma." Tangu kuanzishwa kwake "HabariLEO" limeendelea kujijengea nafasi ya kipekee kama gazeti pekee la Serikali linalochapisha habari kwa Lugha ya Kiswahili, likichangia kukuza matumizi ya Kiswahili na kupeleka habari kwa wananchi wengi zaidi.

Katika kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano, TSN imeendelea kuwekeza katika mageuzi ya kidijitali. Mwaka 2009 "HabariLEO" lilikuwa miongoni mwa magazeti ya

mwanzo nchini kuanzisha tovuti kwa lengo la kuwafikia wasomaji wa ndani na nje ya Tanzania kupitia mifumo ya kidijitali. Tovuti hiyo imeendelea kufanyiwa maboresho makubwa, hasa katika miaka ya 2022 na 2024 ili kuendana na mahitaji ya sasa na ya baadaye ya ulimwengu wa habari za kidijitali.

Sambamba na hilo, TSN imeendelea kuimarisha huduma za "DailyNewsDigital" zinazowezesha wananchi kupata habari kwa wakati kupitia majukwaa ya kidijitali. Hatua hizi zinaonesha dhamira ya kampuni ya kuendelea kubadilika kulingana na mahitaji ya hadhira ya kisasa inayotegemea zaidi teknolojia katika kupata taarifa.

Katika kuendeleza safari hiyo ya mageuzi, TSN pia ipo katika hatua za kuanzisha gazeti la mkononi litakalojulikana kama "TANePress", hatua inayotarajiwa kuleta mapinduzi katika namna wananchi wanavyopata habari kwa njia ya kidijitali kwa haraka na urahisi zaidi, wakati wowote na mahali popote kwa kutumia simu na nyenzo nyingine za kidijitali.

Mbali na "Daily News", "Sunday News" na "HabariLEO", TSN pia imeendelea kupanua wigo wa utoaji wa habari kupitia matoleo ya "East Africa Edition" yanayosaidia kusambaza habari za Tanzania katika ukanda wa Afrika Mashariki na kuimarisha diplomasia ya habari kimataifa. Aidha, kupitia gazeti la michezo la "SpotiLEO",ambalo kwa sasa hupatikana mtandaoni tuu (online edition), kampuni imeendelea kuwafikia wadau wa michezo kwa Taarifa mbalimbali za ndani na nje ya nchi kuhusu soka, riadha, burudani na michezo mingine.

Hata hivyo, mchango wa TSN hauishii katika uchapishaji wa magazeti pekee. Kampuni imeendelea kuwa Taasisi jumuishi inayotoa huduma mbalimbali za kitaalamu katika sekta ya habari, mawasiliano na elimu kwa umma.

Miongoni mwa huduma hizo ni huduma za maktaba na uhifadhi wa nyaraka za kihistoria ambazo zimeifanya TSN kuwa kitovu muhimu cha kumbukumbu za habari nchini. Kwa miongo mingi, kampuni imehifadhi historia na nyaraka mbalimbali muhimu zikiwamo magazeti ya zamani, picha, kumbukumbu za matukio ya kitaifa na nyaraka mbalimbali zinazotumika kama rejea katika tafiti za kitaaluma, kazi za kihabari, na tafiti mbalimbali za maendeleo. Huduma hii imeendelea kuwa msaada mkubwa kwa watafiti, wanafunzi, wanahabari, taasisi za Serikali na wadau wengine wanaohitaji taarifa sahihi za kihistoria.

Kadhalika, TSN imeendelea kujijengea heshima kama kituo cha huduma za kitaalamu za habari (Media Consultancy), kwa kutoa ushauri wa kitaalamu katika uandishi wa habari na mawasiliano kwa umma, kupitia uandishi wa makala maalumu, uandaaji wa maudhui ya taasisi, pamoja na uchakataji wa taarifa kwa taasisi za umma na binafsi. Uzoefu wake wa muda mrefu katika tasnia ya habari umeifanya kampuni kuwa mshirika muhimu kwa taasisi mbalimbali zinazohitaji kuwasiliana kwa ufanisi na umma kwa kuzingatia weledi, usahihi na uwajibikaji.

Katika kuimarisha ushiriki wa wananchi kwenye masuala ya maendeleo ya kitaifa, TSN pia huandaa na kuratibu majukwaa ya utoaji elimu kwa umma (Public Forums) katika maeneo mbalimbali nchini. Majukwa ya Biashara haya hujumuisha washiriki 1,000 hadi 1,500 kutoka taasisi binafsi, za umma, watunga sera na watoa uamuzi wanaojumuika pamoja katika kujadili masuala yanayohusu fursa za biashara na uwekezaji hapa nchini. Washirika na wafadhili wanafurahi kupata fursa ya kukutana na wateja wao ana kwa ana na kujadili masuala yanayowahusu. Pia kupitia majukwaa hayo, taasisi za Serikali, mashirika ya umma na sekta binafsi hupata fursa ya kutoa elimu kuhusu huduma, sera, miradi ya maendeleo, afya, uwekezaji, elimu ya fedha, kilimo, mazingira na masuala mengine muhimu yanayogusa ustawi wa jamii. Majukwaa haya ni nyenzo muhimu na madhubuti ya kujenga uelewa kwa wananchi na kuimarisha mahusiano kati ya taasisi na jamii.

Aidha, TSN inaendelea kutoa huduma za matangazo kupitia magazeti yake pamoja na majukwaa ya kidijitali, hatua inayowezesha taasisi za umma, sekta binafsi na wadau wengine kutangaza bidhaa, huduma, miradi, zabuni, taarifa rasmi na kampeni mbalimbali kwa hadhira pana yenye uaminifu mkubwa. Kupitia nguvu ya magazeti yake pamoja na mifumo ya kidijitali, TSN imeendelea kuwa jukwaa muhimu la mawasiliano nchini.

Sambamba na hayo, TSN inaendelea kuboresha na kutoa huduma za uchapaji wa kibiashara (Commercial Printing), kwa kuboresha miundombinu kwa maana ya majengo ya kiwanda cha uchapaji na ufungaji

wa mitambo mipya na ya kisasa huku ikitumia uzoefu wake wa muda mrefu katika uchapaji kuhudumia taasisi za Serikali, mashirika ya umma, sekta binafsi na wadau wengine wanaohitaji huduma za uchapaji wa nyaraka mbalimbali kwa viwango na ubora wa juu.

Ikiwa na historia ya zaidi ya miaka 90, TSN leo si tu Kampuni ya Magazeti ya Serikali, bali ni Taasisi ya kimkakati yenye weledi katika utoaji wa taarifa sahihi kuhusu ajenda za serikali kwa Wananchi kwa kuzingatia misingi ya ukweli, Kasi, Teknolojia, Ubunifu, Mwitikio na Uwajibikaji, TSN imeendelea kujidhihirisha kama Taasisi inayokwenda sambamba na mabadiliko ya dunia huku ikiendelea kutimiza dhamira yake ya kuhabarisha, kuelimisha na kuunganisha Serikali na jamii kwa maendeleo ya Taifa.

# TSN yapiga hatua uwekezaji wa kisasa miundombinu ya uchapaji



Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) inaendelea kutekeleza mradi mkubwa wa uwekezaji katika miundombinu ya uchapaji unaohusisha ujenzi wa jengo la kisasa la kiwanda cha uchapaji pamoja na ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa.

Akiwasilisha bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, Waziri Paul Makonda alisema hadi sasa ujenzi wa jengo hilo umefikia asilimia 83.1 huku ununuzi wa mitambo ukifikia asilimia 85, hatua inayoonesha ukamilishaji wa mradi uko karibu.

Makonda alisema uwekezaji huo unatarajiwa kuongeza ufanisi na kuboresha ubora wa huduma za uchapaji nchini sambamba na kuimarisha uwezo

wa TSN katika utoaji wa habari na taarifa kwa umma.

Katika eneo la maudhui, TSN imeendelea kuboresha uandaaji na uchapaji wa taarifa kupitia magazeti ya HabariLEO na Daily News pamoja na chaneli ya mtandaoni ya Daily News Digital na majukwaa mbalimbali ya mitandao ya kijamii. Juhudi hizo zinalenga kuhabarisha wananchi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Hadi Aprili 2026, TSN imefanikiwa kuandaa na kuchapisha jumla ya makala za kimkakati 2,973, hatua inayodhihirisha mchango wake katika kuimarisha mawasiliano ya Serikali kwa umma.

Aidha, Waziri Makonda alisema TSN imeendelea kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu za taifa kupitia maktaba maalum ya historia yenye mfumo wa kidijiti. Kupitia mfumo huo, jumla ya matoleo 12,600 ya magazeti ya Daily News na HabariLEO, picha 2,499 pamoja na makala maalumu 2,100 zimewekewa mfumo wa utambuzi (indexing) ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu.

Mfumo huo umehifadhi nyaraka zenye thamani kubwa ya kihistoria ikiwamo historia ya taifa, viongozi wa nchi, harakati za ukombozi wa Kusini mwa Afrika pamoja na masuala ya kidiplomasia. Kutokana na hazina hiyo ya taarifa, TSN imeendelea kuwa chanzo muhimu cha rejea kwa machapisho mbalimbali ya kitaifa na matumizi ya kumbukumbu rasmi za Serikali.

Katika kuimarisha zaidi mifumo ya kidijiti, TSN imeanzisha Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Taarifa (TIMIS) unaounganisha maktaba ya kidijiti na tovuti ya kampuni, hatua inayolenga kurahisisha utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa kwa wadau popote duniani. Kwa ujumla, hatua hizo zinaonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuiwezesha TSN kuwa taasisi ya kisasa, yenye ushindani na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya habari nchini.



# Ubora, weledi waipa TSN Tuzo EJAT-2025



Na mwandishi wetu

KAMPUNI ya Magazeti ya Serikali (TSN) ambayo ni mchapaji wa magazeti ya DailyNews, HabariLEO, SpotiLeo na mitandao ya kijamii ya DailyNews Digital, imeibuka mshindi wa Tuzo ya Chombo Bora cha Habari cha Serikali Kinachotii Sheria Zaidi kwa Mwaka 2025.

Katika hafla ya utoaji wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) iliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na kufanyika Dar es Salaam hivi karibuni, TSN ilitangazwa kuwa ushindi kupitia vigezo vya uzingatiaji wa maadili, utii wa sheria na viwango vya taaluma ya uandishi wa habari.

Mbali na ushindi huo wa TSN kwa ujumla, pia Mhariri wa Habari Msaidizi wa Gazeti la HabariLEO, Halima Mlacha aliibuka na ushindi katika Tuzo ya Uandishi Bora wa Habari za Afya ya Uzazi katika tuzo hizo za msimu wa 16 zinazoandaliwa na MCT.

Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya habari, ushindi wa Halima na TSN kwa ujumla unadhihirisha mchango, ubora na umahiri wa waandishi wa habari wa TSN katika kuibua na kushughulikia masuala ya kijamii.

Wadau wa habari nchini wanazungumzia ushindi wa TSN wakisema Tuzo hizo zinatambua mchango wa kampuni hiyo katika kuzingatia maadili, sheria na viwango vya taaluma ya uandishi wa habari huku ikiendelea kuhabarisha umma ku-

husu masuala mbalimbali ya maendeleo ya taifa.

Mafanikio hayo yanaongeza rekodi ya TSN katika utoaji wa habari za kuaminika kupitia vyombo vyake vya habari.

Akizungumza baada ya TSN kutangazwa na kupokea tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TSN, Asha Dachi alisema huo ni uthibitisho wa namna ambavyo taasisi hiyo imekuwa ikisimamia viwango vya taaluma, maadili na weledi tangu kuanzishwa kwake.

“Hii ni fahari kubwa kwetu…” alisema.

Kwa mujibu wa Dachi, TSN imejijengea heshima kubwa katika tasnia ya habari kwa kuzingatia misingi ya taaluma, sheria na maadili ya uandishi wa habari, huku ikihakikisha dhamira ya kuanzishwa kwa magazeti hayo ya serikali inaendelea kutekelezwa.

Alisema msingi wa mafanikio hayo huanzia katika mchakato wa ajira ambapo waandishi wa habari na watumishi wengine huajiriwa kwa kuzingatia sifa za kitaaluma na taratibu za utumishi wa umma.

Kwa mujibu wa Dachi, baada ya kuajiriwa TSN, watumishi hupatiwa mafunzo na uelekezaji wa kitaaluma kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

“Tunawajenga wanahabari kutambua kuwa wanafanya kazi katika chombo cha habari cha serikali chenye misingi na sera zake,” alisema.

Aliongeza: “Hilo huwasaidia kufanya kazi kwa kuzingatia maadili na viwango vya taaluma.”

Aidha, alimpongeza Halima kwa mafanikio aliyofikia hadi kupata tuzo na kusema ni ushahidi wa uwezo mkubwa uliopo ndani ya TSN.

“Nampongeza Halima kwa kujituma na kuiwakilisha vyema TSN. Ushindi wake unapaswa kuwa chachu kwa wanahabari wengine kushiriki mashindano ya kitaaluma na kupima uwezo wao,” alisema.

Taarifa iliyotolewa awali na Katibu Mtendaji wa MCT na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Tuzo za EJAT, Ernest Sungura ilisema tuzo hizo zinalenga kutambua uandishi bora unaochangia maslahi ya umma, uwajibikaji na mabadiliko chanya katika jamii nchini.

Kwa miaka mingi, TSN imeekuwa sehemu muhimu ya safari ya maendeleo ya taifa kwa kuhabarisha wananchi kuhusu sera za serikali, uchumi, afya, elimu, michezo na masuala mengine muhimu yanayogusa maisha ya kila siku ya Watanzania.

Kupitia mfumo wake wa uandishi unaozingatia ukweli na uwajibikaji, TSN imejijengea heshima na kuaminika miongoni mwa wasomaji wake ndani na nje ya nchi.

Inaelezwa kuwa, mafanikio hayo yanaakisi jitihada za TSN kuimarisha uhusiano mwema na wadau wake kupitia utoaji wa habari sahihi, zilizothibitishwa na zinazojenga uelewa kwa jamii.

Kupitia mkakati wake wa mawasiliano na usimamizi wa taswira ya taasisi, TSN imejenga imani kwa umma kwa kuhakikisha wananchi wanapata taarifa zenye ubora na zinazozingatia maslahi mapana ya taifa.

Katika kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya hadhira ya sasa, TSN pia imeimarisha uwepo wake katika majukwaa ya kidijiti kuhakikisha habari zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa urahisi zaidi.

Hatua hiyo imeongeza wigo wa wasomaji wake na kuifanya iendelee kuwa chanzo muhimu cha habari kwa Watanzania ndani na nje ya nchi.

Kupitia magazeti yake ya HabariLEO, Daily News na SpotiLeo na majukwaa yake ya mtandaoni, TSN imeendelea kutoa habari sahihi, za kuaminika na zenye mchango katika maendeleo ya taifa.

Ushindi katika tuzo za EJAT 2025 unazidi kuimarisha nafasi ya TSN kama taasisi ya habari inayozingatia sheria, maadili na weledi wa taaluma, huku ikibeba dhamana ya kuhabarisha umma kwa uadilifu na uwajibikaji.

# Dkt. Yonazi afanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa TSN

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Dkt. Jim Yonazi amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Bi. Asha Dachi jijini Dodoma kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na mahusiano ya kimkakati baina ya taasisi hizo mbili za Serikali.

Mazungumzo hayo yaliyofanyika tarehe 05 Mei 2026 yalitoa fursa kwa viongozi hao kujadili namna bora ya kuendeleza ushirikiano wenye tija, hususani katika eneo la mawasiliano ya umma, utoaji wa taarifa sahihi kwa wananchi pamoja na matumizi ya majukwaa ya habari katika kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu na vipaumbele vya Serikali.

Kwa upande wake, TSN ilieleza dhamira yake ya kuendelea kuwa mshirika muhimu wa Serikali katika kuhabarisha umma kwa kutumia vyombo vyake vya habari ikiwamo magazeti na majukwaa ya kidijitali ili kuhakikisha ujumbe unaowahusu wananchi unawafikia kwa weledi, usahihi na kwa kuzingatia maadili ya taaluma ya habari. Vilevile, kikao hicho kilionesha umuhimu wa kuendeleza ushirikiano unaolenga kukuza mawasiliano ya taasisi za umma kwa manufaa ya wananchi na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Aidha, mazungumzo hayo yalilenga kujenga mshikamano wa kiutendaji utakaochochea uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utoaji wa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari vya Serikali.



# PSSSF na TSN kuimarisha ushirikiano wa kimkakati katika utendaji.



Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umeahidi kuimarisha ushirikiano wa kimkakati na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) katika utekelezaji wa majukumu ya serikali kwa lengo la kufikia wateja wake.

Akizungumza katika kikao kilichofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya TSN, Meneja wa PSSSF Kanda ya Temeke, Bi. Maria Lupondo alisema amefurahishwa na taarifa aliyoipata kutoka kwa Menejimenti ya TSN kutokana na ufafanuzi wa majukumu yanayotekelezwa na TSN.

“Sikuwahi kujua kuwa TSN mnatekeleza majukumu makubwa kiasi hiki, sisi tunajua kuwa TSN ni wachapaji wa magazeti tu,kumbe bado mna shughuli nyingi mnafanya nje ya uchapaji wa magazeti. PSSSF kuna kazi nyingi za kufanya na TSN sasa naomba tufanye kazi kimkakati hasa katika uchapaji wa nyaraka mbalimbali ambazo ni nyenzo za uelemishaji,” alisema Bi. Lupondo.

Naye Bi. Coletha Mnayamani ambaye ndio alikuwa mkuu wa msafara, alisema PSSSF ipo tayari kutumia majukwaa ya kidigitali ya TSN pamoja na kupata ushauri wa kitaalamu katika kuhabarisha umma kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na PSSSF.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi wa Habari wa TSN, Bw. Majaliwa Christopher aliwaeleza ni kwa namna gani TSN inaweza kutumia majukwaa yake kufikisha taarifa sahihi kwa umma na kwa wakati hasa elimu na huduma mbalimbali zinazotolewa na mfuko huo wa hifadhi ya jamii nchini .

Aidha, alifafanua umahiri na uzoefu wa TSN katika masuala ya habari huku akiwahakikishia maofisa hao ufanisi katika utekelezaji wa makubaliano ambayo yatatekelezwa kwa wakati na kwa kiwango watakavyokuwa wamekubaliana katika mkataba kwani matokeo ya kazi yataleta tija kwa pande zote mbili .

“TSN pamoja na majukumu mengine lakini suala la kusukuma ajenda za serikali ili zifikie jamii kwa mapana yake ni jukumu letu, hivyo tuendelee kushirikiana na tupotayari kwa utekelezaji naamini ziara hii ya leo italeta manufaa makubwa, kwani imeongeza hari kwa TSN kwakuwa kuja kwenu hapa kumeongeza kujuana zaidi,” alisema Bw. Majaliwa.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara TSN, Bi. Soter Salema alielezea maeneo ya kimkakati yatakayokuwa fursa muhimu kwa ushirikiano wa kikazi. Miongoni mwa maeneo hayo ni uzinduzi wa gazeti mkononi litakalofahamika kama TANePres, majukwaa ya kutoa elimu kwa umma,

huduma za maktaba, majukwaa ya kidijitali, huduma za uchapaji pamoja na huduma za ushauri wa kitaalamu katika masuala ya uandishi wa habari.

Kikao hicho kimetokana na ziara iliyofanywa na maofisa uhusiano waliotembelea TSN kwa lengo la kuongeza mahusiano pamoja na kujifunza namna TSN inavyotekeleza majukumu yake.

# TSN yashiriki Mei Mosi



Watumishi wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) wameshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja kwa Mkoa wa Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya kuenzi mchango wa wafanyakazi katika maendeleo ya taifa na kuhimiza uwajibikaji mahali pa kazi.

Maadhimisho hayo yaliwakutanisha wafanyakazi kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi, viongozi wa Serikali pamoja na wadau wa sekta mbalimbali ambapo ujumbe mkuu ulikuwa kuendelea kuthamini nguvu kazi ya Watanzania na mchango wao katika uchumi na maendeleo ya nchi.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila ambaye aliwahimiza wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii, maarifa na kujituma kwa hali ya juu ili kuchangia ujenzi wa taifa imara na lenye maendeleo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mheshimiwa Chalamila alisema; “Nawaomba kila mtumishi, awe wa sekta ya umma au binafsi, kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kujenga nchi yetu na kufikia mafanikio chanya katika sekta zote. Kaulimbiu ya mwaka huu wa Mei Mosi inajieleza vyema, na ninaamini kila mmoja ataizingatia”.

Aidha, aliwataka waajiri kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na kuhakikisha wafanyakazi wanapata haki zao za msingi pamoja na mazingira salama yatakayowezesha kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi .

Kwa upande wake, TSN imeendelea kuonesha dhamira yake ya kuthamini mchango wa wafanyakazi wake kwa kuimarisha mazingira ya kazi, kukuza taaluma na kuhamasisha ushirikiano miongoni mwa watumishi ili kuongeza ubunifu na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Ushiriki wa TSN katika maadhimisho hayo pia umeakisi nafasi ya taasisi hiyo katika kuhabarisha

umma, kuelimisha jamii pamoja na kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuhimiza maendeleo endelevu kupitia sekta ya habari na mawasiliano.

Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani huadhimishwa kila mwaka tarehe 1 Mei. Kwa mwaka huu, maadhimisho ya kitaifa yamefanyika mkoani Njombe yakihudhuriwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa mgeni rasmi.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni; "Kazi zenye Staha ni Nguzo Imara kwa Maendeleo Endelevu katika Utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050," ikiwa inalenga kuhimiza ushiriki wa wafanyakazi katika kujenga uchumi endelevu kupitia kazi yenye tija, uwajibikaji na maadili memaya kazi.

# Dachi awasihi Wanafunzi nidhamu na matumizi sahihi ya AI



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Bi. Asha Dachi amewasihi wanafunzi wa kidato cha sita wa Shule ya Sekondari Zanaki kuwa na nidhamu, kujifunza bila kikomo pamoja na kuwa na uthubutu katika masomo yao ili wafikie ndoto na malengo yao ya baadaye.

Bi. Dachi alitoa wito huo wakati akizungumza na wanafunzi, walimu na wazazi katika mahafali ya kidato cha sita yaliyofanyika katika Shule ya Sekondari Zanaki jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo, alisema dunia ya sasa imejaa mabadiliko makubwa ya kiteknolojia, hususan matumizi ya akili unde (Artificial Intelligence - AI), hivyo vijana wanapaswa kuwa makini na kuitumia teknolojia hiyo kwa njia sahihi na yenye manufaa kwa maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.

"Niwaombe kuzingatia maadili ya Kitanzania na kujenga nidhamu katika maisha yenu ya kila siku. Upande mwingine unaohitaji umakini wa hali ya juu ni matumizi ya teknolojia ya akili unde. Teknolojia hii imeleta mabadiliko makubwa hata katika namna tunavyofanya kazi. Kwa namna nyingine unaweza ukaona ni tishio kwa hatma ya ajira, lakini pia tunaweza kuichukua kama nyenzo muhimu ya kusaidia jamii yetu," alisema Bi. Dachi.

Aliongeza kuwa pamoja na maendeleo hayo ya

teknolojia, wanafunzi wanapaswa kuendelea kujijengea uwezo wa kufikiri, kufanya tafiti na kutumia maarifa yao binafsi badala ya kutegemea teknolojia kufanya kila jambo kwa niaba yao.

“Nami leo tunapomaliza hapa na kwenda vyuoni, tusiitumie akili unde kujibu maswali kwa kutegemea kila kitu kutoka huko. Ina uwezo mkubwa wa kujibu maswali ukiingiza swali, lakini hutakuwa umejisaidia kujenga uwezo wako binafsi. Tunatakiwa tujenge uwezo wetu, ubinadamu wetu na fikra zetu ili tuwe wataalamu wenye mchango chanya katika jamii,” alisisitiza.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kuwa na uthubutu wa kujaribu fursa mbalimbali zinazojitokeza katika maisha yao ya kitaaluma na kijamii, huku wakizingatia maadili, heshima na uwajibikaji.

Bi. Dachi pia aliipongeza shule hiyo kwa kuendelea kufanya vizuri katika taaluma na malezi ya wanafunzi wa kike, jambo ambalo limeendelea kusaidia kuwaandaa wasichana kuwa viongozi na wataalamu wa baadaye katika sekta mbalimbali nchini.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari Zanaki, Bi. Delvine Koka alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi wa kike 1,175 kuanzia kidato cha kwanza hadi sita, ikiwa na walimu 60 pamoja na watumishi wasio walimu sita.

Alisema pamoja na mafanikio yanayopatikana kitaaluma na kinidhamu, shule hiyo bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ubovu wa sakafu za vyumba vya madarasa, upungufu wa kompyuta za kufundishia, ukosefu wa viyoyozi (AC) pamoja na uchakavu wa viti vya wanafunzi.

Bi. Koka alitoa wito kwa wadau wa elimu, taasisi na jamii kwa ujumla kuendelea kushirikiana na shule hiyo katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora inayokidhi mahitaji ya dunia ya sasa.

Mahafali hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa elimu, wazazi, walezi pamoja na wageni waalikwa, ambapo wahitimu walikumbushwa umuhimu wa kuendelea kuwa mabalozi wazuri wa shule yao na taifa kwa ujumla kupitia nidhamu, juhudi na uwajibikaji katika kila hatua ya maisha yao.



# Watumishi TSN wapatiwa mafunzo ya Mpango Mkakati 2026 –2030



Watumishi wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) wamepatiwa mafunzo maalumu yaliyolenga kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi kwa kipindi kijacho cha miaka mitano 2026–2030 ikiwa ni sehemu ya kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma.

Semina hiyo ya siku tano kuanzia tarehe 20 hadi 24 April, 2026 iliendeshwa na Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Tathmini na Ufuatiliaji, Bw. Joseph Moshi katika Makao Makuu ya kampuni hiyo yaliyopo Tazara jijini Dar es Salaam.

Katika mafunzo hayo, Bw. Moshi alifafanua kwa kina utekelezaji wa majukumu ya taasisi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, akieleza malengo, mikakati na vipaumbele vinavyotarajiwa kuzingatiwa ili kuongeza tija, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa kila siku.

Alisema Mpango Mkakati wa TSN wa Miaka Mitano 2026 –2030 umeandaliwa kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia, mahitaji ya soko la habari pamoja na dira ya taasisi ya kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi kupitia vyombo vyake vya habari.

“Ni muhimu kila mtumishi kuelewa nafasi yake katika utekelezaji wa mpango mkakati huu ili kuhakikisha taasisi inaendelea kufikia malengo yake kwa ufanisi. Ushirikiano, uwajibikaji na ubunifu vitakuwa msingi mkubwa wa mafanikio yetu katika kipindi hiki kijacho,” alisema Bw. Moshi.

Aidha, aliwataka watumishi kuzingatia matumizi sahihi ya rasilimali za taasisi pamoja na kuendelea kuimarisha utendaji kazi unaozingatia maadili ya utumishi wa umma.

Mbali na mafunzo hayo, watumishi pia walipatiwa mafunzo maalumu kuhusu mpango wa kuongeza ujuzi kwa lengo la kuboresha huduma za taasisi kwa mujibu wa Muongozo wa Utumishi wa Umma (Training Needs Assessment - TNA).

Mafunzo hayo yaliwasilishwa na Ofisa Rasilimali watu wa TSN, Bi. Edna Mahimbo, ambaye alieleza umuhimu wa watumishi kuendelea kujifunza, kujiendeleza kitaaluma na kuongeza ujuzi unaoendana na mabadiliko ya teknolojia na mazingira ya kisasa ya kazi.

Bi. Mahimbo alisema kuwa maendeleo ya teknolojia pamoja na mabadiliko ya mifumo ya utoaji hudu-

ma yanahitaji watumishi kuwa tayari kujifunza kila wakati ili kuongeza ushindani na ubora wa kazi zao.

“Tunapaswa kuhakikisha watumishi wetu wanakuwa na ujuzi unaohitajika katika kipindi hiki cha mabadiliko ya kidijitali ili taasisi iweze kuendelea kutoa huduma bora na zenye tija kwa jamii,” alisema.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yataendelea kuwa sehemu muhimu ya mkakati wa taasisi katika kuwajengea watumishi uwezo na kuwawezesha kufanya kazi kwa weledi zaidi.

Kwa upande wao, baadhi ya watumishi walioshiriki semina hiyo walieleza kuwa mafunzo hayo yamewasaidia kuelewa kwa undani zaidi mwelekeo wa taasisi pamoja na namna bora ya kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia malengo ya TSN kwa miaka ijayo.

Semina hizo zilitolewa kwa vitengo na kurugenzi zote za TSN, hatua inayolenga kuhakikisha kila mtumishi anakuwa sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati wa taasisi kwa pamoja.

Kupitia mafunzo hayo, TSN inaendelea kuonesha dhamira yake ya kuwekeza katika rasilimali watu kwa kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuongeza ubora wa huduma, ubunifu na ushindani katika sekta ya habari na mawasiliano nchini.



# BIDHAA NA HUDUMA ZETU

## 1. MAGAZETI

Kampuni inachapisha magazeti manne (4) mashuhuri na yanayotegemewa zaidi nchini katika lugha za Kiingereza na Kiswahili. Magazeti ya Kiingereza ni Daily News na Sunday News. HabariLEO ni gazeti la Kiswahili la kila siku na SpotiLeo ni gazeti la kila wiki la michezo la Kiswahili. Kampuni inachapisha majarida manne (4) ya Kiingereza na manane (8) ya kila wiki ya Kiswahili, Majarida ya lugha ya Kiingereza ni Business Standard, Academy, Woman, na Score,wakati majarida ya lugha ya Kiswahili ni; "JamiiYetu", "Ulingo wa Siasa", "Elimika", "Maarifa", "Urithi Wetu", "Nyota", "Penalti Box" na "Frii Kiki". Majarida hayo yanalenga makundi maalum ya wasomaji




## 2. UCHAPAJI WA KIBIASHARA

Kampuni inatoa huduma za uchapishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo majarida, kalenda, vipeperushi (brochures), vijitabu (booklets), daftari za kumbukumbu (diaries), machapisho ya taarifa (newsletters), magazeti, vipeperushi vya matangazo (leaflets), aina zote za flyers, notepads za matangazo, prospectus, uchapishaji wa screen printing, huduma za branding (magari, vikombe, miamvuli n.k.), bendera ndogo za mkononi (hand flags), T-shirt, mugs, bahasha, kadi za salamu, mabango (posters), stika pamoja na uuzaji wa karatasi za A4 (rim paper).



## 3. HUDUMA ZA USHAURI WA MAWASILIANO NA HABARI

Kampuni inatoa ushauri wa kitaalamu katika eneo la vyombo vya habari na huduma za utangazaji kwa lengo la kujenga taswira chanya ya shirika au taasisi lengwa. Huduma hii inahusisha utengenezaji wa vipindi vya elimu kwa umma kupitia redio, televisheni, mitandao ya kijamii na Makala za magazeti na pia kutengeneza miongozo ya mawasiliano kama vile Sera na Mikakati ya Mawasiliano ili kuziwesha taasisi zinazotaka huduma hii kuwa na mifumo rasmi ya mawasiliano na hivyo kupunguza athari au hasara zitokanazo na changamoto za kimawasiliano baina ya wafanyakazi, Menejimenti na wadau.



## 4. MATANGAZO

Katika dunia ya leo, mafanikio yanategemea ama kuzalisha bidhaa au kutoa huduma. Wajibu wetu ni kuhakikisha bidhaa au huduma zako zinawafikia walengwa kwa ufanisi kupitia huduma zetu za matangazo. Tunatangaza biashara yako kupitia vyombo vyetu vya habari, ikiwemo magazeti yanayopatikana katika nakala za kuchapishwa na majukwaa ya mtandaoni, ili kuhakikisha ujumbe wako unawafikia wateja wengi zaidi ndani na nje ya nchi.



## 5. JUKWAA LA BIASHARA

Jukwaa la Biashara ni mkutano unaowakutanisha wadau mbalimbali kujadili masuala yenye maslahi ya kitaifa, sera na ajenda za maendeleo zinazolenga kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii nchini.

Majukwaa haya yamewahi kufanyika katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Lindi, Tanga, Zanzibar, Tabora, Geita, Arusha, Pwani na Shinyanga. Kwa wastani, jukwaa hushirikisha washiriki kati ya 1,000 hadi 1,500 kutoka taasisi za umma na binafsi, balozi na ofisi za kidiplomasia, pamoja na wananchi kwa ujumla, kwa lengo la kujenga mitandao na kujadili masuala yanayohusu biashara na uwekezaji.

Washirika na wadhamini wa jukwaa hupata fursa ya kukutana na wateja wao watarajiwa na waliopo kupitia mawasilisho ya biashara, utambulisho wa chapa (branding), maonyesho ya bidhaa na huduma, pamoja na shughuli za kujenga mitandao ya kibiashara (business networking).



## 6. E-PAPER (Gazeti Mtandao)

E-Paper ni moja ya bidhaa zetu mpya inayokua kwa kasi nchini. Kupitia huduma hii, unaweza kupata gazeti zima kwa njia ya mtandao kwa gharama nafuu na kwa haraka zaidi kulinganisha na nakala ya gazeti la kuchapishwa.

Huduma hii hufanya matangazo yako yaonekane kwa wakati, kuwafikia wasomaji wengi zaidi, na kukuwezesha kupata habari kwa haraka popote ulipo.

Unaweza kupata huduma ya E-Paper kwa kujisajili kupitia mfumo rahisi na kuanza kufurahia upatikanaji wa habari wakati wowote: epaper.tsn.go.tz.



TANZANIA STANDARD NEWSPAPERS

DAILY NEWS • HabariLEO • sundaynews • DAILY NEWS

tsn_corporate
habarileo_tz
dailynews_tz
HabariLeo
Daily News Tanzania
HabariLeo
dailynewstz
DailyNews Digital

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
Kampuni ya Magazeti ya Serikali

Makao Makuu: Barabara ya Nelson Mandela
PostiKodi 15102, Jengo la Daily News, KitaluNa. 11/4
S.L.P 9033, Dar Es Salaam
Namba ya simu: +255 222 864 863
Barua Pepe:barua@tsn.go.tz